

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA

(BaruaazoteziandikwekwaMkurugenziMtendaji)

MKOA WA DODOMA

Simu: 255 -026-2320537

Fax No. : 255-026-2320537

E-Mail: dedkongwa@gmail.com



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P. 57,
KONGWA.

Kumb. Na. HW/KOG/S. 20/29.VOL. IV/69

Tarehe 23/03/2018

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa anawatangazia nafasi za kazi Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi za Watendaji wa Vijiji kwa Masharti ya Kudumu.Tangazo hili ni baada ya kupokea kibali cha ajira mbadala chenye Kumb. Na. CFC 26/205/01 “F”/91 cha tarehe 22/08/2017, Pamoja na barua ya nyongeza ya muda wa utekelezaji kibali cha ajira mbadala kwa Watendaji wa Vijiji na Mitaa yenye Kumb Na. CFC.26/205/01”GG”/95 ya tarehe 12, Machi, 2018 zote kutoka kwa Katibu Mkuu (UTUMISHI).

Mchanganuo wa nafasi ni kama ifuatavyo:-

1. MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III - (NAFASI 33)

SIFA

Mwenye Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliye hitimu mafunzo ya Astashahada /Cheti” Technician Certificate”(NTA LEVEL 5) katika moja ya fani zifuatazo:-

Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

MAJUKUMU

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- ii. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.

- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananachi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa , umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa wakuu wa vitengo nya kitaalam katika kijiji.
- viii. Kusimamia kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za vijiji.
- ix. Kutekeleza shughuli nyingine atakazopangiwa na mwajiri wake.

NGAZI YA MSHAHARA

Mshahara ni kwa mujibu wa viwango nya mshahara Serikalini yaani **TGS B** sawa shilingi za kitanzania **390,000/=** kwa mwezi.


MASHARTI YA JUMLA

- 2. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa.
- 3. Mwombaji awe na umri kati ya Miaka 18 na usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
- 4. Maombi yote, ya waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (detailed CV),Namba za simu na anuani sahihi.
- 5. Maombi yote ya waombaji yaambatane na nakala za vyeti nya taaluma, vyeti nya elimu ya Kidato cha (IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (Passport size) na iandikwe jina nyuma.
- 6. Testimonials “Provisional results” “Statement of results” hati ya matokeo ya kidato cha Nne na Sita **HAVITAKUBALIWA**.
- 7. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU na NECTA) na taarifa ya uhakiki iambatanishwe kwenye maombi.
- 8. Siku ya usaili kila mwombaji afike na vyeti halisi nya Elimu, Taaluma, Kuzaliwa na Kitambulisho.
- 9. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba, isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

10. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
11. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 05, Aprili, 2018, Saa 9:00 alasiri.
12. Barua zote ziandikwe kwa mkono wa mwombaji na kutumwa kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji ,
Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa
S.L.P. 57,
KONGWA

N.B Masharti yaliyoanishwa kwenye tangazo hili yasomwe kwa makini na yazingatiwe.


NGUSA L. IZENGO
MKURUGENZI MTENDAJI (W)

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
S.L.P. 57
KONGWA

- Nakala.** Katibu Tawala (M)
" Katibu Tawala (W)
" Halmashauri zote za Mkoa wa Dodoma
" Mbao za Matangazo
" Waheshimiwa Madiwani wote
" Watendaji wa Kata Wote